

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano limeundwa kisheria chini ya kifungu cha 37 cha Sheria ya Mamlaka Ya Mawasiliano Na. 1 2 ya mwaka 2003 kwa madhumuni ya kulinda na kutetea maslahi na haki za mtumiaji wa huduma za mawasiliano Tanzania.

**ANUANI
YETU**

**BARAZA LA USHAURI
LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA
MAWASILIANO TANZANIA**

Baraza la ushauri la watumiaji wa
huduma za mawasiliano
Jengo la Wizara ya Ujenzi,
Uchukuzi na Mawasiliano, Ghorofa ya 2
14 Mtaa wa Jamhuri
S.L.P 1516
11470 Dar es salaam, Tanzania
Simu : +255 22 212 2691/2
+255 652 966 633
Barua pepe : info@tcra-ccc.go.tz
Tovuti : www.tcra-ccc.go.tz



**BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI
WA HUDUMA ZA MAWASILIANO
TANZANIA**

**SHERIA YA MAKOSA YA
MTANDAO YA MWAKA
2015**

UTANGULIZI

Sheria ya makosa ya mtandao inaainisha makosa na adhabu zinazohusiana na matumizi ya mfumo wa kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Ukuaji wa kasi wa Teknolojia ya Habari na mawasiliano na Matumizi yake nchini Tanzania yamepelekea umuhimu wa sheria hii kukabiliana na makosa yatoakanayo na matumizi ya mtandao.

Utendaji makosa wa kwenye mtandao ni tofauti na makosa yanayofanyika na kusimamiwa na sheria nyingine. Makosa ya mtandao siyo lazima yafanyike ndani ya mipaka ya kijiografia ya nchi husika na siyo lazima kitu kilichoibwa kihamishike

Sheria zilizopo hazitambui makosa yanayofanyika kwenye mtandao hivyo kupelekea vyombo vya maamuzi kushindwa kutekeleza wajibu wake. Ili mtu adhibiwe kisheria ni lazima kosa liainishwe kwenye kanuni za adhabu au litambulike kisheria ndipo mtu anaweza kutiwa hatiani.

Kwa kutambua hilo Bunge la Jamhuri ya Muungano lilipitisha sheria ya Makosa ya Mtandao tarehe 1 aprili 2015 na kuridhiwa na Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 25 Aprili, 2015.

MASUALA MUHIMU KWENYE SHERIA

- (i) Utoaji na ukusanyaji wa maudhui katika data
- (ii) Ponografia
- (iii) Ponografia ya watoto
- (iv) Utoaji wa taarifa za uongo
- (v) Ujumbe unaotumwa bila ridhaa
- (vi) Matusi ya kibaguzi
- (vii) Mauaji ya kimbari na makosa dhidi ya ubinadamu
- (viii) kuzuia upelelezi
- (ix) Unyanyasaji kupitia mtandao
- (x) Ukiukaji wa haki bunifu
- (xi) Kula njama ya kutenda kosa
- (xii) Ulinzi wa miundombinu muhimu ya TEHAMA

AINA ZA MAKOSA YA MTANDAO

- (1) Makosa dhidi ya Usiri, Usalama na Upatikanaji wa taarifa za kompyuta na mifumo ya kompyuta mathalani kuingilia mawasiliano ya kompyuta au mifumo ya kompyuta kinyume cha sheria, wizi wa taarifa kimtandao
- (2) **Makosa dhidi ya kutumia Kompyuta ni pamoja na :**
 - (i) Udanganyifu kwa kutumia kompyuta
 - (ii) Kugushi kwa kutumia kompyuta
 - (iii) Wizi wa utambulisho wa mtu binafsi mtandaoni
 - (iv) Matumizi ya vifaa kinyume cha sheria
- (3) **Makosa yanayohusiana na Maudhui kama vile :**
 - (i) Usambazaji wa ponografia
 - (ii) Ponografia ya watoto
 - (iii) Kashfa na taarifa za uongo
 - (iv) Makosa dhidi ya ubaguzi wa rangi na chuki
 - (v) Michezo ya kamari mitandaoni kinyume cha sheria
 - (vi) Makosa dhidi ya Haki na Hati miliki
- (4) Sheria inatambua muungano wa makosa kama vile utakatishaji wa fedha haramu na ugaidi kwa kutumia mtandao

ADHABU DHIDI YA UKIUKWAJI WA SHERIA

Aina ya Kosa	Adhabu Dhidi ya Ukiukwaji wa Sheria
Udanganyifu Unaohusiana na kompyuta	Faini isiyopungua Sh. Milioni 20 au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria au kifungo kisichopungua miaka 7 au vyote kwa pamoja.
Wizi wa utambulisho wa mtu binafsi mtandaoni	Faini isiyopungua Sh. Milioni 5 au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria au kifungo kisichopungua miaka 7 au vyote kwa pamoja.
Kutoa taarifa za uongo	Faini isiyopungua Sh. Milioni 5 au kifungo kisichopungua miaka 3 au vyote kwa pamoja.
Ponografia ya watoto	Faini isiyopungua Sh. Milioni 50 au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria au kifungo kisichopungua miaka 7 au vyote kwa pamoja.
Ponografia	<ul style="list-style-type: none"> ● Uchaphishaji wa ponografia : Faini isiyopungua Sh. Milioni 20 au kifungo kisichopungua miaka 7 au vyote kwa pamoja. ● Ponografia chafu au ya kiasherati : faini isiyopungua sh. Milioni 30 au Kifungo kisichopungua miaka 10 au vyote kwa pamoja
Unyanyasaji kwa kupitia mtandao	Faini isiyopungua Sh. Milioni 5 au kifungo kisichopungua miaka 3 au vyote kwa pamoja.
Ujumbe unaotumwa bila ridhaa (usambazaji wa ujumbe unaotumwa bila ridhaa, kurusha tena au kusambaza upya ujumbe unaotumwa bila ridhaa, kugushi ujumbe wa utambulisho na kutuma bila ridhaa). taarifa bila ridhaa ni kutuma taarifa au data kieletroniki bila kuombwa na mpokeaji	Faini isiyopungua Sh. Milioni 3 au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria au zaidi au kifungo kisichopungua miaka 1 au vyote kwa pamoja.